GLOBAL NETWORK FOR
Social Justice &
Digital Resilience

# SCANNING THE HORIZON

Mustakabali
wa Haki za Kidijitali
na Ustahimilivu kwa
Wengi wa Dunia

GLOBAL NETWORK FOR
Social Justice &
Digital Resilience

digitalresilience.network

**KUCHUNGUZA HORIZONI**
Mustakabali wa Haki za Kidijitali
na Ustahimilivu kwa Wengi wa Dunia

Ripoti hii, iliyoandikwa na **Juan Ortiz Freuler**, iliagizwa na Mtandao wa Kimataifa wa Haki za Kijamii na Ustahimilivu wa Kidijitali (DRN) kwa lengo la kuchunguza mwelekeo wa siku zijazo na masuala husika yanayolikabili ekolojia ya haki za kidijitali na ustahimilivu wa kidijitali katika nchi za Kusini mwa Dunia. Haionyeshi lazima mitazamo na maoni ya wanachama wa DRN.


Mwandishi: Juan Ortiz Freuler
Wahariri: Paulina Gutiérrez, Lidija Sabados, Claudio Ruiz
Mhariri wa Lughai: Adriana Sánchez
Wabunifu wa Muundo: Comunas Unidas

Tarehe ya Kuchapishwa Mara ya Kwanza: Machi 2024
Imesasishwa: Februari 2025

Agencya ya ukalimani: Tranzlati Global
(Makao makuu Yako Lagos, Nigeria)
Tovuti: www.tranzlati.com



Kazi hii inapatikana chini ya leseni ya Creative Commons Attribution 4.0 Kimataifa.
https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/deed.en

# JEDWALI LA MAUDHUI


4 I. DIBAJI

5 II. UTANGULIZI

6 III. MWELEKEO KATIKA UTAWALA WA DUNIA, JIOPOLITIKI, NA HALI MPYA ZA KISIASA ZA KIENEO
Uchanganuzi
Muktadha
Mielekeo
Kuchipuka kwa miungano mipya ya kibiashara na athari zake kwa utawala wa dunia
Deni la umma linapunguza nguvu ya majadiliano
Siasa za ndani katika muktadha wa uhaba: kuongezeka kwa dhaifu na matumizi mabaya
Matarajio Ya Baadaye

17 IV. MIELEKEO YA TEKNOLOJIA
Uchanganuzi
Muktadha
Mielekeo
Kuunganishwa kwa ngazi zote za miundo ya mtandao
Kupinga uaminifu na kutoa upya
Uwekaji wa data kienyeji
Matarajio Ya Baadaye

26 V. MIELEKEO INAYOATHIRI UANAHARAKATI
Uchanganuzi
Muktadha
Mielekeo
Muungano na mashirika ya kiraia ya haki za binadamu
Mabadiliko katika agenda ya wafadhili na kuongezeka kwa changamoto za kupata fedha
Changamoto na fursa mpya kwa wanaharakati unaotegemea teknolojia
Matarajio Ya Baadaye

34 VI. HITIMISHO

# I.
# DIBAJI

Ulioanzishwa mwaka 2021, Mtandao wa Kimataifa wa Haki za Kijamii na Ustahimilivu wa Kidijitali unaundwa na washirika kumi waliobobea wanaofanya kazi kwa ushirikiano katika maeneo ya walio wengi duniani, kwa lengo la kuimarisha ustahimilivu wa kidijitali wa mfumo wa haki za kijamii. Lengo kuu la mtandao huu ni kuzalisha na kushiriki maarifa pamoja na kushiriki katika michakato ya fikra bunifu ambayo hujenga na kufundisha mbinu za pamoja za kuimarisha uwezo wa kiteknolojia wa kila mshirika wake na hatimaye kuimarisha ustahimilivu wa kidijitali na mfumo wa haki za kijamii kwa ujumla.

Muhtasari huu unaleta pamoja na kuendeleza taarifa na maarifa yaliyokusanywa kupitia mahojiano na wanachama wa mtandao pamoja na wajumbe wa bodi ya ushauri, kuanzia Novemba 2023 hadi Machi 2024. Lengo la zoezi hili lilikuwa kusaidia kundi hili kutambua fursa na changamoto ambazo uwanja wa haki za kidijitali utakumbana nazo katika muongo ujao, na jinsi vipengele hivyo vitakavyoathiri ekolojia ya haki za kidijitali na ustahimilivu wa kidijitali kwa ujumla. Matokeo yetu ya pamoja pia yatatumika kuendeleza ajenda ya mtandao yenye mtazamo wa baadaye.

Badala ya kuichukulia ripoti hii kama taswira kamili na ya mwisho ya changamoto na fursa zijazo katika uwanja huu, hati hii ilikusudiwa kuwa msingi wa majadiliano na maendeleo ya kudumu. Hapo awali ilibuniwa kama zoezi la ndani, lakini wanachama wa mtandao waliamua kushiriki matokeo yao na wadau wengine kwa upana zaidi, kwa nia ya kuanzisha majadiliano ya asili na kuwaalika washiriki wengine wa mfumo huu kutafakari na kujenga juu ya maarifa yaliyomo humu.

# II.
# UTANGULIZI

Mustakabali si jambo lisilotabirika tu, bali pia unaweza kubadilishwa. Katika miongo iliyopita, mashirika ya kiraia yamefanikiwa kuathiri mijadala ya umma, kanuni za udhibiti, na jinsi teknolojia za kidijitali zinavyofanya kazi. Mwelekeo mbalimbali ambao utaiathiri sekta hii katika muongo ujao utahitaji kuzingatiwa na mashirika hayo — kuanzia kuporomoka kwa mifumo ya ikolojia na uhamaji mkubwa wa watu, hadi mabadiliko katika utawala wa kimataifa na dunia inayozidi kuwa ya kidijitali.

Hati hii inalenga kuchochea na kuelekeza mazungumzo kuhusu muktadha ambao utahusisha utetezi wa haki za kidijitali na ustahimilivu wa kidijitali katika siku zijazo. Kwa madhumuni ya ripoti hii, haki za kidijitali zinarejelea ulinzi na uendelezaji wa haki za binadamu katika mazingira ambamo teknolojia za kidijitali zinabadilisha maisha ya binadamu. Kwa mtazamo wa kiufundi, ustahimilivu wa kidijitali utatumika kumaanisha uwezo wa teknolojia za kidijitali kuendelea kufanya kazi kama zana salama na zenye manufaa kwa watetezi wa haki za kijamii wanaozitegemea katika kuendeleza kazi yao[1]. Muhtasari huu unalenga kuchangia majadiliano katika makutano ya ajenda hizi mbili. Hasa zaidi, unalenga kutoa mchango katika juhudi hizi kwa mtazamo na maadili ya Kusini mwa Dunia, ukimulika baadhi ya mazingira mahususi ambayo mashirika katika maeneo haya huenda yakakumbana nayo katika miaka ijayo. Ni matarajio yetu kwamba mazungumzo kama haya yataongeza uwezo wa mashirika haya kutambua mapema hatari au kufaidika na mfumo wa kidijitali pamoja na mashirika ya kiraia yaliyo ndani yake.

Ripoti hii inajengwa juu ya mahojiano yaliyofanywa na takriban watendaji 20 wa haki za binadamu na haki za kidijitali, pamoja na utafiti wa mezani na uchambuzi wa data, ili kutoa mtazamo wa baadaye kuhusu maeneo matatu muhimu: serikali na jiografia ya kisiasa, teknolojia, na harakati za kijamii.




**Mielekeo ya Kiteknolojia**
1. Uwekaji wa Mamlaka Kituo Kimoja na Uimarishaji
2. Sheria Dhidi ya Ukiritimba
3. Uwekaji wa Data Ndani ya Nchi

**Mielekeo ya Siasa za Kijiografia na Siasa za Ndani ya Eneo**
1. Sanduku Jipya la Biashara
2. Deni Lisilodumu
3. Uhaba wa Ndani na Mvutano wa Kijamii

**Mielekeo katika Uanaharakati**
1. Muunganiko na Ajenda Pana ya Haki za Binadamu
2. Mabadiliko ya Vipaumbele vya Wafadhili
3. Mizunguko ya Zana za Kiteknolojia kwa ajili ya Uanaharakati

Kwa kila nguzo iliyobainishwa hapo juu, muhtasari huu unashughulikia yafuatayo:

- nguvu kuu zinazounda muktadha,
- mitazamo inayoendelea ambayo huenda ikaathiri sekta hii katika miaka ijayo, na
- hali mbalimbali zinazoweza kuibuka kutokana na mchakato huu ambazo zinaweza kutoa msingi wa pamoja kuelekea maono ya pamoja ya siku zijazo.

1. Kwa mjadala mpana zaidi kuhusu tafsiri ya ustahimilivu wa kidijitali kama inavyoshughulikiwa na Mtandao, tazama: https://digitalresilience.network/how-do-we-define-digital-resilience/

# III. MWELEKEO KATIKA UTAWALA WA DUNIA, JIOPOLITIKI, NA HALI MPYA ZA KISIASA ZA KIENEO

## A. UCHANGANUZI

- **Ushindani kati ya Marekani na China unaathiri upatikanaji wa teknolojia:** Ushindani kati ya Marekani na China unaweza kuathiri masharti ambayo yatadhibiti jinsi nchi za Kusini mwa Dunia zitakavyopata teknolojia au uhamishaji wa teknolojia. Mchakato huu utaathiri kiwango ambacho teknolojia itaendeleza au kuzuia haki za binadamu na masilahi ya watu wa Kusini mwa Dunia, pamoja na mazingira ya taarifa ambamo mijadala kuhusu changamoto hizi inafanyika.

- **Uratibu kati ya pembezoni unakuwa wa dharura:** Viwango vya juu vya madeni ya umma vinaweza kupunguza uwezo wa nchi kujadiliana kwa niaba ya wananchi wao katika mifumo ya kimataifa ya taarifa na uchumi. Uratibu kati ya nchi au kanda zilizo pembezoni unakuwa muhimu zaidi ili kuongeza nguvu ya majadiliano kwa kila mshiriki.

- **Kupungua kwa nafasi ya kiraia kutokana na shinikizo za kiuchumi na kijamii:** Mazingira magumu ya kiuchumi yanazidi kudhoofisha imani kwa serikali, jambo linaloweza kuongeza migogoro na kupunguza zaidi nafasi ya kiraia. Mashirika ya kiraia huenda yakakumbana na changamoto mpya katika utekelezaji wa shughuli zao za kila siku. Hali hii inahitaji marekebisho ya mikakati ya ushirikishwaji wa umma, upatikanaji wa rasilimali, na vipengele vingine vinavyosaidia ustahimilivu wa mashirika.

## B. MUKTADHA

- **Pengo linalozidi kuongezeka kati ya mamlaka na uwajibikaji:** Mtandao wa intaneti umoja mawasiliano ya wakati halisi kwa kiwango cha dunia. Kuanzia ushairi hadi vita, ufundishaji hadi biashara mawasiliano yetu yote sasa yamejikita kwenye itifaki ya mtandao. Kwa hivyo, intaneti ni teknolojia yenye uwezo wa kubadili mfumo wa utawala wa dunia. Hata hivyo, wakati biashara na utoaji wa huduma vimekuwa vya kimataifa, mifumo yetu ya kisiasa haijafikia kiwango hicho, hali inayosababisha haki na uhuru wa binadamu mtandaoni kuwa jambo la pili au la tatu kwa umuhimu, huku mtandao unaolenga biashara ukiendelea kukua. Mifumo yetu ya utawala wa dunia[2] haijakua sambamba na athari wala kasi ya soko hili la kimataifa. Pengo hili linaloongezeka kati ya mahali mamlaka ilipo na mahali taasisi za kuiwajibisha zilipo linaweza kueleza mvutano mingi tunayoshuhudia leo.

- **Shinikizo linalotokana na hali hii kwa mifumo ya utawala:** Ndani ya nchi, pengo hili linachochea migogoro na kudhoofisha uaminifu kwa wawakilishi wa umma ambao wanaonekana kushindwa kutoa majibu kwa migogoro ya ndani, huku imani kwa serikali ikizidi kuporomoka kwa kasi katika nchi za kidemokrasia katika miaka ya hivi karibuni[3]. Katika ngazi ya kimataifa, hali hii inaangazia mapungufu ya muundo wa sasa wa utawala wa dunia[4]. Kwa maneno ya Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa: "Katiba ya Umoja wa Mataifa

---

2. Mifumo ya utawala wa dunia inarejelea mifumo au mbinu ambazo mapenzi ya watu yanaweza kutafsiriwa kuwa sera katika kiwango cha kimataifa. Mfano wa kawaida ni Umoja wa Mataifa, lakini kuna mashirika mengine ya ngazi ya kikanda (kama vile Umoja wa Afrika, Shirika la Nchi za Amerika) pamoja na mashirika maalum ya eneo fulani kama vile Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) na Shirika la Biashara Duniani (WTO) ambayo pia yana nafasi katika michakato hii iwe kwa manufaa au kwa hasara.

3. Edelman, "2022 Edelman Trust Barometer," Edelman, 2022, https://www.edelman.com/trust/2022-trust-barometer; Manuel Castells, Rupture: The Crisis of Liberal Democracy (Cambridge, UK; Medford, MA: Polity Press, 2018).

4. Stewart Patrick, "Rules of Order: Assessing the State of Global Governance" (Carnegie Endowment for Peace, 12 Septemba, 2023), https://carnegieendowment.org/2023/09/12/rules-of-order-assessing-state-of-global-governance-pub-90517.

na maadili inayoyawakilisha yako hatarini... tumejikita katika hali ya kutofanya kazi kwa kiwango kikubwa duniani"[5]. Hitilafu hii inaonekana si tu kwa kushindwa kuwawajibisha mataifa yenye nguvu, bali pia kwa kushindwa kudhibiti mamlaka yanayotekelezwa na makampuni binafsi ya kiteknolojia ya kimataifa ambayo yanazidi kuwa na ushawishi mkubwa[6]. Matokeo yake ni kwamba changamoto kama mabadiliko ya tabianchi na uhamaji wa kulazimishwa, pamoja na usimamizi wa mifumo yetu ya kimataifa ya taarifa, zimekuwa vigumu sana kukabiliana nazo.

- **Mabadiliko makubwa ya jiopolitiki:** Mvutano kati ya Marekani na China—mataifa yenye uchumi mkubwa zaidi na viongozi katika ubunifu wa kiteknolojia—ni miongoni mwa mabadiliko makuu tunayoshuhudia katika safu ya utawala wa dunia. Mtandao wa intaneti uliingia kwa kasi katika ulingo wa kimataifa wakati wa enzi ya dunia yenye mhimili mmoja katika miaka ya 1990, na tangu wakati huo, kiwango chake cha kupokelewa duniani kimeendelea kuongezeka kwa kasi kubwa. Kwa hivyo, ni vigumu kwa wengi wetu kutenganisha matarajio yetu juu ya teknolojia hii na misingi ya kiliberali pamoja na simulizi la "mwisho wa historia" ambamo ilikua. Wakati mwaka 1994, Makamu wa Rais wa Marekani Al Gore alikuwa akiuelezea mtandao kama "barabara kuu ya mawasiliano ambayo watu wote wataisafiri"[7], ifikapo mwaka 2020, Waziri wa Mambo ya Nje wa zamani Mike Pompeo alikuwa akitoa wito kwa nchi kujiunga na Mtandao Safi, ambao ungewatenga wapinzani wa Marekani[8]. Mchanganyiko wa utegemezi unaoongezeka kwa teknolojia za taarifa, hatua ya Marekani kuachana na biashara huria na (neo)liberalism[9], pamoja na mchakato unaoendelea kuelekea dunia ya mihimili miwili au mingi, utaathiri kwa kiasi kikubwa jinsi tunavyopata teknolojia, kushiriki taarifa, na kwa upana zaidi, namna tunavyoshiriki katika majukwaa ya utawala wa dunia na uchumi wake. Kwa hivyo, kuna mwelekeo mitatu inayopaswa kupewa kipaumbele maalum na wadau wanaofanya kazi katika masuala ya haki za kidijitali na ustahimilivu wa kidijitali.

5. António Guterres, "Hotuba ya Katibu Mkuu kwa Baraza Kuu" (Umoja wa Mataifa, 20 Septemba 2022), https://www.un.org/sg/en/content/sg/speeches/2022-09-20/secretary-generals-address-the-general-assembly.

6. Katika baadhi ya matukio, taasisi hizi hata zimekuwa zikikuza nafasi ya sekta binafsi katika mijadala ya kimataifa na mazungumzo ya kidiplomasia, jambo ambalo linapunguza kwa kiasi kikubwa nafasi ya mataifa na mashirika ya kiraia.

7. Al Gore, "VP Remarks at the International Telecommunications Union," 1994, https://web.archive.org/web/20010528184855/https://clinton1.nara.gov/White_House/EOP/OVP/html/telunion.html.

8. US Department of State, "The Clean Network," United States Department of State (blog), Agosti 2020, https://2017-2021.state.gov/the-clean-network/.

9. This is meant to be a description of a context in which there will be a weakened rhetoric for free flow in general: Free flow of goods, free flow of money, free flow of people, free flow of information. For more background on this change, see Matthew Duss and Ganesh Sitaraman, "The Era of Neoliberal U.S. Foreign Policy Is Over," Foreign Policy (blog), December 27, 2023, https://foreignpolicy.com/2023/05/18/neoliberal-foreign-policy-biden-sullivan/; Gary Gerstle, The Rise and Fall of the Neoliberal Order: America and the World in the Free Market Era, 1st ed. (Oxford University Press, 2022), https://doi.org/10.1093/oso/9780197519646.001.0001.

## C. MIELEKEO

### KUCHIPUKA KWA MIUNGANO MIPYA YA KIBIASHARA NA ATHARI ZAKE KWA UTAWALA WA DUNIA

Wakati nchi nyingi za Kusini zinauza malighafi muhimu kwa kiwango kikubwa, nyingi kati yao huagiza teknolojia zinazohitajika kushiriki katika mazingira ya kidijitali. Kama inavyoonyeshwa kwenye Mchoro wa 1 hapa chini, mahusiano mengi ya kikoloni na ya baada ya ukoloni kati ya Kaskazini na Kusini bado yanaendelea kuwepo. Ni nchi chache tu ambazo jirani yao ndiye mshirika wao mkuu wa kibiashara, huku bara la Ulaya likibakia kuwa mshirika mkuu wa biashara kwa nchi nyingi za Afrika, na Marekani ikiendelea kuwa na ushawishi mkubwa katika Amerika ya Kati na kaskazini mwa Amerika ya Kusini[10].

- **Kuchipuka kwa BRICS:** Nchi za BRICS (Brazil, Urusi, India, China na Afrika Kusini) zinazidi kuwa muhimu katika ngazi ya kimataifa. Ingawa washirika wadogo kama Brazil na Afrika Kusini wanaonyesha ushawishi wao wa kikanda, China imekuwa mshirika mkuu wa kibiashara kwa nchi nyingi za Kusini mwa Dunia, ikiwa chanzo kikuu cha uagizaji kwa nchi nyingi za Amerika Kusini na Asia. Zaidi ya hayo, kupanuka kwa BRICS kujumuisha nchi muhimu zinazouza nishati kama Saudi Arabia, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), na Iran (pamoja na Misri na Ethiopia) kunaweza kuongeza ushawishi wa wanachama wa BRICS katika eneo la MENA[11], uwezo wao wa kuunda upya mifumo ya biashara ya kimataifa kwa upana zaidi[12], na kupunguza utegemezi wa dola ya Marekani katika biashara hiyo ya kimataifa[13]. Maendeleo haya yana uwezo wa kuyumbisha mizani ya kibiashara ya kimataifa, na athari zake zinaweza kugusa mifumo ya kisheria na kisiasa ya nchi wanachama wa BRICS na zile zilizo karibu nazo, zikiwemo kampuni zinazotoa teknolojia, jambo linaloweza kuleta changamoto na fursa mpya kwa uendelezaji wa haki za binadamu.

---

**10.** To see how the main trading partners evolved over the past decades, see https://twitter.com/sundellviz/status/1488596964208001026.

**11.** Alkesh Sharma, "Saudi Arabia and China Sign Deals Worth $25bn to Boost Economic Ties," The National, December 12, 2023, https://www.thenationalnews.com/business/economy/2023/12/12/saudi-arabia-and-china-sign-deals-worth-25bn-to-boost-economic-ties/.

**12.** Sumayya Ismail, "'A Wall of BRICS': The Significance of Adding Six New Members to the Bloc," Al Jazeera, August 24, 2023, https://www.aljazeera.com/news/2023/8/24/analysis-wall-of-brics-the-significance-of-adding-six-new-members; Julian Borger, "Brics to More than Double with Admission of Six New Countries," The Guardian, August 24, 2023, sec. Business, https://www.theguardian.com/business/2023/aug/24/five-brics-nations-announce-admission-of-six-new-countries-to-bloc.

**13.** Rachel Savage and Rachel Savage, "What Is a BRICS Currency and Is the U.S. Dollar in Trouble?," Reuters, August 24, 2023, sec. Currencies, https://www.reuters.com/markets/currencies/what-is-brics-currency-could-one-be-adopted-2023-08-23/; Robert Greene, "The Difficult Realities of the BRICS' Dedollarization Efforts—and the Renminbi's Role," Carnegie Endowment for International Peace (blog), December 5, 2023, https://carnegieendowment.org/2023/12/05/difficult-realities-of-brics-dedollarization-efforts-and-renminbi-s-role-pub-91173.

*Mchoro 1: Chanzo namba moja cha uagizaji na usafirishaji wa bidhaa kwa nchi mbalimbali duniani (2022)*[14]

**UINGIZAJI KUTOKA**



**USAFIRISHAJI KWENDA**



Soko Kuu la Usafirishaji/ Uagizaji Bidhaa

- Brazili
- Urusi
- India
- China
- Afrika Kusini
- Umoja wa Ulaya
- Marekani

---

**14.** Chanzo: Imetayarishwa na mwandishi kwa kutumia takwimu kutoka Shirika la Biashara Duniani Toleo la mwingiliano linapatikana hapa. Tanbihi: Mnamo Februari 2024, ilitangazwa kuwa Marekani sasa ina Mexico kama chanzo chake kikuu cha uagizaji bidhaa. https://www.npr.org/2024/02/08/1229965009/mexico-has-overtaken-china-as-the-leading-source-of-goods-imported-to-the-u-s.

- **Kutengana Kwa Marekani Na China Na Miale Yake Kwa Ustahimilivu Wa Kidijitali:** Ingawa Marekani na China zimeunda mtandao uliofungamana wa uzalishaji wa viwandani katika miongo iliyopita[15], wanasiasa wa Marekani wanaongeza shinikizo kwa kampuni na nchi nyingine kujitenga na China. Katika eneo la teknolojia za kidijitali, hili lilionekana kupitia mpango wa Clean Network ulioendelezwa na Waziri wa Mambo ya Nje wa zamani Mike Pompeo wakati wa utawala wa Trump[16], na baadaye kuingizwa rasmi katika sera za serikali chini ya utawala wa Biden kupitia Chips Act[17] na sera za friendshoring zinazopigiwa debe na Waziri wa Hazina Janet Yellen[18], zilizofuata mlolongo wa vikwazo dhidi ya kampuni kuu za China kama Huawei[19]. Kwa hivyo, Marekani imekuwa ikizishinikiza waziwazi serikali mbalimbali kuukataa Huawei barani Ulaya, Amerika ya Kusini[20], Afrika na maeneo mengine[21], huku Marekani ikiwekeza katika kuunda miundombinu mbadala ya 5G[22] ili kufidia pengo.

Mwelekeo huu unaweza kusababisha vikwazo katika upatikanaji wa watoa huduma mbadala wa teknolojia (na kufungua mianya kwa mifumo ya biashara ya unyonyaji zaidi), lakini pia unaweza kupelekea uhamishaji mkubwa wa teknolojia kutoka katika vituo vya nguvu huku vikishindana kwa ushawishi katika nchi za Kusini. Kuimarisha uwezo wa majadiliano wa nchi ndogo na za kati kwa kuratibu mikakati ya pamoja ya mazungumzo kutakuwa muhimu ili kusukuma mbele ajenda za kitaifa na kikanda.

---

15. Richard Baldwin, Rebecca Freeman, na Angelos Theodorakopoulos, "Hidden Exposure: Measuring U.S. Supply Chain Reliance" (Brookings Institute, September 2023), https://www.brookings.edu/wp-content/uploads/2023/09/2_Baldwin-et-al_unembargoed.pdf; Anshu Siripurapu na Noah Berman, "The Contentious U.S.-China Trade Relationship," Baraza la Mahusiano ya Kigeni (blogu), Septemba 26, 2023, https://www.cfr.org/backgrounder/contentious-us-china-trade-relationship.

16. Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani, "The Clean Network."

17. White House, "FACT SHEET: CHIPS and Science Act," The White House (blog), Agosti 9, 2022, https://www.whitehouse.gov/briefing-room/statements-releases/2022/08/09/fact-sheet-chips-and-science-act-will-lower-costs-create-jobs-strengthen-supply-chains-and-counter-china/.

18. Janet Yellen, "Remarks by Secretary of the Treasury Janet L. Yellen at Microsoft in New Delhi, India" (US Department of the Treasury, Novemba 11, 2022), https://home.treasury.gov/news/press-releases/jy1096.

19. Ana Swanson, "U.S. Delivers Another Blow to Huawei With New Tech Restrictions," The New York Times, Mei 15, 2020, sec. Business, https://www.nytimes.com/2020/05/15/business/economy/commerce-department-huawei.html.

20. Andres Schipani, Jude Webber, and Benedict Mander, "Latin America Resists US Pressure to Exclude Huawei," FT.Com, 2019, https://search.proquest.com/docview/2237413242?pq-origsite=primo.

21. Mathieu Pollet and John Hendel, "The West Is on a World Tour against Huawei," POLITICO, Novemba 28, 2023, https://www.politico.eu/article/west-world-tour-huawei-china-telecom/.

22. Ina Fried, "U.S. to Spend $1.5 Billion to Jumpstart Alternatives to Huawei," Axios, Desemba 7, 2022, https://www.axios.com/2022/12/07/huawei-alternatives-5g-cellural-equipment-oran.

## 1. DENI LA UMMA LINAPUNGUZA NGUVU YA MAJADILIANO

Kipengele muhimu kinachoathiri nguvu ya majadiliano ni uwezo wa mhusika kusubiri hadi masharti yanayofaa yajitokeze. Nchi ikiwa na uwezo wa kukopa, haihitaji kutegemea biashara kupata sarafu ngumu za kuagiza teknolojia na bidhaa nyingine ambazo haziwezi kuzalishwa ndani ya nchi. Hata hivyo, changamoto kubwa kwa nchi nyingi katika suala hili ni viwango vya juu vya deni la umma.

- **Viwango vya deni vinaendelea kuwa juu kulinganisha na Pato la Taifa (GDP):** Njia mojawapo ya kupima uhimilivu wa deni ni kulinganisha na Pato la Taifa (GDP), ambalo hupima thamani ya soko ya bidhaa na huduma zote zinazozalishwa nchini kwa kipindi fulani, mara nyingi mwaka mmoja[23]. Deni la umma duniani limeongezeka mara tatu tangu miaka ya 1970, na kufikia mwisho wa mwaka 2022 lilikuwa limefikia 92% ya GDP[24].

*Mchoro wa 2: Deni kama asilimia ya Pato la Taifa (2023 au makadirio ya hivi karibuni)*[25]

**Deni kwa Pato la Taifa**




**23.** Kuna mambo ya kati muhimu yanayoathiri uwezo wa nchi kuchukua deni zaidi, ambayo kwa msingi wake hufafanuliwa na kiwango cha imani ambacho wadau wengine wanaweza kuwa nacho kuhusu uwezo wa nchi hiyo kulilipa deni hilo, au jukumu la kimkakati ambalo uhimilivu wa mpango wa kiuchumi unaweza kuwa nalo kwa nchi nyingine. Uchambuzi wa kina zaidi wa uhimilivu wa deni huangazia mwingiliano wa muda mrefu kati ya viwango vya deni kwa Pato la Taifa (GDP), mapato na matumizi ya serikali, na mizania ya biashara ya nje. Uchambuzi zaidi wa kina unapatikana kupitia sehemu ya marejeleo: IMF, "Global Debt Monitor," 2022, https://www.imf.org/-/media/Files/Conferences/2022/12/2022-12-12-global-debt-monitor.ashx; Neil R. Mehrotra and Dmitriy Sergeyev, "Debt Sustainability in a Low Interest Rate World," Journal of Monetary Economics, The Real Interest Rate and the MarginalProduct of Capital in the XXIst Century Oktoba 15–16, 2020, 124 (Novemba 1, 2021): S1–18, https://doi.org/10.1016/j.jmoneco.2021.09.001; Nouriel Roubini, "Debt Sustainability: How to Assess Whether a Country Is Insolvent" (NYU Stern School of Business, 2001).

**24.** IMF, "Global Debt Is Returning to Its Rising Trend," IMF, Septemba 13, 2023, https://www.imf.org/en/Blogs/Articles/2023/09/13/global-debt-is-returning-to-its-rising-trend.

**25.** Chanzo: Kimeandaliwa na mwandishi kwa kutumia data kutoka CIA Factbook. Data inaonyesha makadirio ya hivi karibuni zaidi, mara nyingi kutoka mwaka wa 2023. Toleo shirikishi linapatikana kwa kubofya kwenye ramani.

Kama inavyoonyeshwa na mchoro wa 2 (hapo juu), nchi nyingi zimevuka kiwango cha 50% (kwa rangi nyekundu), huku nchi kama India, Brazil, Argentina, Venezuela, Zimbabwe, Misri na nyingine nyingi zikiwa na deni la umma lililovuka 80% ya GDP yao. Kama itakavyofafanuliwa katika sehemu inayofuata, mbali na kupunguza uwezo wao wa kujadiliana katika masoko ya kimataifa na hivyo kupunguza fursa ya kupata teknolojia kwa haki viwango vya juu vya deni la umma vinaweza kuongeza migogoro ya kijamii na kiuchumi ndani ya nchi.

## 2. SIASA ZA NDANI KATIKA MUKTADHA WA UHABA: KUONGEZEKA KWA DHAIFU NA MATUMIZI MABAYA

Wakati benki kuu za mataifa zinatekeleza ongezeko kubwa la viwango vya riba ili kukabiliana na mfumuko wa bei, nchi za pembezoni zinashuhudia kupungua kwa uwekezaji wa nje na kuondoka kwa sarafu ngumu kutoka katika nchi zao kuelekea kwenye hati fungani za Hazina ya Marekani na mali nyingine zinazochukuliwa kuwa salama zaidi kwa uwekezaji, kwa kuwa mapato yake yanakuwa yanazidi kuvutia[26].

Matokeo ya mchanganyiko huu wa ukosefu wa upatikanaji wa mikopo na upungufu wa uwekezaji wa kigeni, ni kwamba nchi zilizozama kwenye madeni hukimbilia sera kali za kubana matumizi, ambazo hujumuisha kupunguza matumizi ya umma mara nyingi huacha idadi kubwa ya watu bila huduma muhimu kama vile chakula, elimu, huduma za afya, pensheni, dawa, na mengine mengi[27]. Utafiti wa mwaka 2022 ulikadiria kuwa ndani ya miezi 12, asilimia 85 ya watu duniani wanaoishi katika nchi 143 wangekuwa wakiishi chini ya hatua za kubana matumizi[28].

Kwa sababu ya sera za kubana matumizi, ukosefu wa usawa huongezeka na sehemu kubwa ya wananchi huachwa wakihisi kutoweza kushiriki kikamilifu au kwa haki katika maisha ya umma, hali inayochochea kutokuamini serikali[29], maandamano[30], na katika baadhi ya matukio, ukandamizaji, huku viongozi wa kisiasa wakijaribu kuimarisha mamlaka yao katika mazingira yaliyogawanyika kwa kudhoofisha uwezo wa wakosoaji kujieleza. Kama inavyoonyeshwa kwenye ramani hapa chini (Mchoro 3), udhaifu wa taasisi katika sehemu kubwa ya nchi za walio wengi duniani tayari uko katika viwango vya juu sana, jambo linalomaanisha kuwa uwezo wa serikali kushughulikia changamoto zilizobainishwa katika muhtasari huu tayari ni mdogo.

**26.** Anna Cooban, “Why You Should Care about the Global Rout in Government Bonds | CNN Business,” CNN, October 4, 2023, https://www.cnn.com/2023/10/04/business/global-bond-market-sell-off-explainer/index.html; Tobias Adrian, “Higher-for-Longer Interest Rate Environment Is Squeezing More Borrowers,” IMF (blog), Oktoba 10, 2023, https://www.imf.org/en/Blogs/Articles/2023/10/10/higher-for-longer-interest-rate-environment-is-squeezing-more-borrowers.

**27.** Oxfam, “The 2022 Commitment to Reducing Inequality (CRI) Index,” Oxfam International, Oktoba 19, 2022, https://www.oxfam.org/en/research/2022-commitment-reducing-inequality-cri-index.

**28.** Matti Kohonen and Isabel Ortiz, “Austerity: A Raging Storm for the Developing World That Can Be Avoided,” Inter Press Service, Oktoba 24, 2022, sec. Economy & Trade, https://www.ipsnews.net/2022/10/austerity-raging-storm-developing-world-can-avoided/.

**29.** Edelman, “2022 Edelman Trust Barometer”.

**30.** Abubakr Al-Shamahi, “How Economic Hardship Fuelled the Arab Spring 10 Years Ago,” Al Jazeera, 2022, https://www.aljazeera.com/news/2020/12/17/bread-and-gas-economic-boost-needed-after-arab-spring.

*Mchoro wa 3: Kiashiria cha Nchi Zenye Udhaifu wa Taasisi*[31]




31. Chanzo: Imetayarishwa na mwandishi kwa kutumia data kutoka Fragile States Index, inayofadhiliwa na kituo cha tafakuri cha Marekani, Fund for Peace. Toleo la mwingiliano linapatikana kwa kubofya ramani.

Kama ilivyoainishwa na Shirika la Fund for Peace, nchi za kipato cha kati zinaonyesha mifumo inayofanana na ile ya baada ya mzozo wa kifedha wa mwaka 2008, huku bei za chakula zikipanda katika kipindi cha miaka minne iliyopita, zaidi ya watu milioni 250 katika nchi 58 wakikumbwa na uhaba mkubwa wa chakula mwaka 2022, na zaidi ya nchi 90 zikishuhudia maandamano kuhusu mafuta[32]. Zaidi ya kulemea mashirika yasiyo ya kiserikali kwa changamoto za kiutawala, kibinafsi, na kitaaluma, mvutano huu unaweza kusababisha ongezeko la matumizi mabaya ya teknolojia za kidijitali na serikali ili kukandamiza haki za msingi za binadamu, kama vile uhuru wa kujieleza na wa kukusanyika.

Kwa mfano:

- **Kuongezeka kwa idadi ya vizuizi vya mtandao:** Mnamo mwaka 2022, tulishuhudia rekodi ya mataifa 35 yaliyotekeleza vizuizi vya mtandao, na jumla ya vizuizi kufikia 187[33].

- **Udukuzi na ufuatiliaji uliosambaa:** Pia tunaona matumizi ya mbinu za ufuatiliaji zinazotumia upatikanaji mpana wa vifaa vya mkononi ili kufikia maeneo ya faragha kabisa. Mnamo mwaka 2021, nyaraka zilizovuja zilionyesha kuwa simu za watu wapatao 50,000 zilikuwa kwenye rada ya mteja mmoja wa kampuni ya programu ya ujasusi ya NSO Group[34]. Mwelekeo huu pia umetajwa katika moduli kuhusu uanaharakati, ikieleza udhaifu wa baadhi ya zana za msingi ambazo sasa ni muhimu kwa kuandaa harakati na kampeni za mabadiliko.

Mchanganyiko wa hali hizi na mitazamo hii unaonyesha uwezekano wa aina mbalimbali za mustakabali ambazo mashirika ya kiraia yanayopigania haki za kidijitali na uimara wa kidijitali yanapaswa kuzingatia wanapopanga kazi yao kwa miaka ijayo.

---

**32.** Fund for Peace, "Fragile States Index 2023," 2023, https://fragilestatesindex.org/wp-content/uploads/2023/06/FSI-2023-Report_final.pdf.

**33.** Zach Rosson et al., "Internet Shutdowns in 2022: The #KeepItOn Report," Access Now (blog), 28 Februari 2023, https://www.accessnow.org/internet-shutdowns-2022/.

**34.** Stephanie Kirchgaessner et al., "Revealed: Leak Uncovers Global Abuse of Cyber-Surveillance Weapon," The Guardian, 18 Julai 2021, sec. Habari za dunia, https://www.theguardian.com/world/2021/jul/18/revealed-leak-uncovers-global-abuse-of-cyber-surveillance-weapon-nso-group-pegasus.

## D. MATARAJIO YA BAADAYE

Mwelekeo mkuu uliowasilishwa katika moduli hii ni mabadiliko katika utawala wa kimataifa, ambayo yanaweza kusababisha harakati kuelekea:

- **Dunia yenye nguvu nyingi (multipolar):** Marekani inajiondoa kwenye msimamo wa kibepari (ikiwa na msukumo mdogo wa kuunga mkono uhuru wa usafirishaji wa bidhaa, pesa, watu na data), huku China (ikiwa na mtazamo wa kisiasa na kiuchumi unaoongozwa zaidi na serikali) ikizidi kupata ushawishi katika ulingo wa kimataifa kwa kufanya makubaliano na viongozi wa kikanda, kama kupitia muungano wa BRICS, na kuongeza ushawishi wake katika taasisi kama Umoja wa Mataifa[35]. Kutokana na hali hiyo, huenda dunia ikaelekea kuwa ya nguvu nyingi zenye tofauti kubwa katika sera na mazingira ya habari yaliyo na utofauti zaidi hata kama migogoro ya mtandaoni itaongezeka.

- **A Ulimwengu wa Ncha Mbili:** Iwapo juhudi za BRICS[36] na nyinginezo zilizopo[37] (au zijazo) za kubadilisha namna utawala wa kimataifa unavyofanya kazi zitashindwa, dunia inaweza kuelekea katika hali ya kuwa na ncha mbili, ambapo China na Marekani zitadhibiti kwa ukaribu taarifa na teknolojia zinazozunguka ndani ya maeneo yao ya ushawishi. Katika hali hiyo, mataifa ya pembezoni yanaweza kuwa maeneo ya majaribio ya teknolojia, silaha za mtandaoni na mbinu nyingine za kuathiri ajenda za kisiasa katika baadhi ya nchi.

- **Unipolar Ulimwengu wa Ncha Moja:** Vinginevyo, tunaweza kuendelea au kuimarisha zaidi hali ya dunia yenye ncha moja. Hii inaweza kupunguza migogoro, lakini pia inaweza kupunguza uhuru katika mataifa ya pembezoni na kusababisha ufanano mkubwa zaidi wa teknolojia na taarifa.

- **More Ulimwengu usio na utawala wa kutosha:** Hatimaye, tunaweza kufikiria hali ambapo changamoto za kuongoza dunia inayozidi kuwa na muunganiko mkubwa zinashinda hata uwezekano wa kuwa na ulimwengu wa ncha moja. Hii inaweza kusababisha mifumo na mabaraza yaliyopo ya utawala wa kimataifa kuporomoka, na hivyo kuwa na utofauti mkubwa wa sera, kupungua kwa uwezo wa kutekeleza sheria kimataifa, na kuongezeka kwa migogoro ya mtandaoni baina ya na ndani ya kanda mbalimbali.

---

**35.** Jeffrey Feltman, "China's Expanding Influence at the United Nations — and How the United States Should React" (Brookings Institute, 2020), https://www.brookings.edu/wp-content/uploads/2020/09/FP_20200914_china_united_nations_feltman.pdf.

**36.** Niall Duggan et al., "Introduction: 'The BRICS, Global Governance, and Challenges for South–South Cooperation in a Post-Western World,'" International Political Science Review 43, no. 4 (1 Septemba, 2022): 469–80, https://doi.org/10.1177/01925121211052211.

**37.** David Adler, "The West v Russia: Why the Global South Isn't Taking Sides," The Guardian, March 28, 2022, sec. Opinion, https://www.theguardian.com/commentisfree/2022/mar/10/russia-ukraine-west-global-south-sanctions-war; Marco A. Vieira, "Understanding Resilience in International Relations: The Non-Aligned Movement and Ontological Security," International Studies Review 18, no. 2 (2016): 290–311, https://www.jstor.org/stable/24758593.

Swali muhimu kwa muktadha wa ustahimilivu wa kidijitali ni jinsi mchakato wa kutunga kanuni za kimataifa unaosimamia mfumo wa sasa wa taarifa duniani utakavyobadilika katika muongo ujao.

Mwelekeo huu unaweza kuchorwa kama ifuatavyo.




Zoezi lenye manufaa kwa wasomaji na timu zao linaweza kuwa kujadili mahali tulipo kwenye ramani iliyopendekezwa kwa sasa, ni wapi mitazamo ya sasa inaweza kutupeleka katika kipindi cha miaka kumi ijayo, na athari gani mabadiliko hayo yatakuwa nayo:

1. *Je, itakuwa na athari gani kwa teknolojia na jamii kwa ujumla?*

2. *Ni aina gani za shughuli ambazo sekta inapaswa kuanza kuzifanyia kazi sasa ili kuendeleza hali ambayo inafaa zaidi kulinda haki za kidijitali na haki za binadamu kwa ujumla?*

3. *Mikakati, tamko la dhamira, na ustahimilivu wa jumla wa taasisi utaathiriwaje na mabadiliko hayo?*

# IV.
# MIELEKEO YA TEKNOLOJIA

## A. UCHANGANUZI

- **Madaraka yanazidi kukusanywa mikononi mwa kampuni chache tu:** Mchakato huu wa kuunganishwa unaweza kuzidi kupunguza uwezo wa wanaharakati, serikali, na mifumo ya utawala ya kimataifa kufuatilia kikamilifu na kuhakikisha kuwa teknolojia zinaheshimu haki za binadamu na kuendeleza maslahi ya umma.

- **Sheria za kupinga ukiritimba katika nchi kuu za teknolojia zinatoa tumaini la mabadiliko:** Uchunguzi kadhaa unaoendelea Marekani, China, na kwingineko unatoa mwanga wa matumaini, na unaweza kubadilisha kabisa taswira ya wachezaji wakuu wa teknolojia.

- **Sera za kuweka data ndani ya mipaka ya nchi huenda zikawa za kawaida:** Serikali zinazojali faragha, mamlaka ya kitaifa, na ukosefu wa mifumo ya kuwawajibisha kampuni za kigeni zinaanza kulazimisha kampuni kubwa za kimataifa kuhifadhi vituo vya data na mali nyingine ndani ya mipaka yao.

## B. MUKTADHA

Teknolojia mbalimbali zimevutia umakini mkubwa wa umma, ikiwa ni pamoja na akili bandia (AI), hali halisi pepe (VR), blockchain, kompyuta za kwanta, na huduma za intaneti kupitia satelaiti, miongoni mwa nyingine. Badala ya kujaribu kufafanua utafiti mpana uliopo kuhusu mizunguko ya matumaini na kuvunjika moyo kuhusu teknolojia mpya, sehemu hii itajikita zaidi katika suala kuu la madaraka[38], ambalo linajitokeza katika kila teknolojia mpya kwa kuonyesha ni nani atakuwa na nafasi ya kuielekeza na kufaidika nayo.

**Mitandao ya kijamii kama mfano wa unyakuzi wa mamlaka ya kampuni:** Ili kueleza jinsi mtoa huduma ya teknolojia anavyoweza kutumia na kuongeza mamlaka yake katika uwanja wa taarifa, hebu tuchunguze mitandao ya kijamii. Hizi ni majukwaa ambayo wengi wetu tumekuwa tukitumia kila siku kwa zaidi ya muongo mmoja, na yaliyokuwa na mabadiliko makubwa kiasi cha kuitwa “mtandao wa kijamii wa kizazi cha pili” (web 2.0). Ingawa kampuni hizi za mitandao ya kijamii zimehifadhi (kwa kiasi kikubwa) majina yao ya awali, vipengele na tabia za majukwaa haya zimebadilika sana kwa miaka kadhaa, na hivyo kuwawezesha wasimamizi wake kutumia madaraka makubwa zaidi katika uwanja wetu wa taarifa, wakielekeza uwezo wetu wa kujieleza na kupata maarifa kwa kiwango ambacho hakijawahi kushuhudiwa katika historia. Mabadiliko haya, kwa ujumla, yanaonyesha unyakuzi wa mamlaka wa kiwango kikubwa.

**38.** Gartner, “4 Exciting New Trends in the Gartner Emerging Technologies Hype Cycle,” Gartner (blog), 23 Agosti 2023, https://www.gartner.com/en/articles/what-s-new-in-the-2023-gartner-hype-cycle-for-emerging-technologies.

*Jedwali 1. Ukuaji wa mamlaka yanayotekelezwa na kampuni za mitandao ya kijamii juu ya uwanja wetu wa taarifa*

| HATUA | VIPENGELE MUHIMU VYA JUKWAA | UPEO WA UAMUZI WA WASIMAMIZI | ATHARI ZA HIARI YA MAJUKWAA | NGUVU INAYOTUMIWA NA MAJUKWAA |
|---|---|---|---|---|
| 2004 – 2006 | Orodha ya mawasiliano yenye wasifu. **Kuchapisha maudhui kwenye wavuti kumerahisishwa.** “Democratization” of blogs. | **Imepunguzwa:** Wanaondoa maudhui na profaili zinazokiuka masharti na vigezo. | **Chini:** Watumiaji wachache ambao –kwa wastani– hutumia muda mchache mtandaoni. | **Chini** |
| 2006 – 2009 | Maudhui ambayo kila mtumiaji huchapisha kwenye wasifu wake huzalisha nakala ambayo huwa wazi kwa mtandao wa mawasiliano katika **nafasi ya kati** ambapo maudhui hupangwa kwa mpangilio wa muda. Hii hupunguza hitaji la mtumiaji kusogeza kwa mikono kutafuta maudhui. | **Imepunguzwa:** Huwa wanaondoa maudhui na wasifu vinavyokiuka masharti na vigezo vya huduma. | **Chini:** Watumiaji chini ya bilioni 1, ambao –kwa wastani– hutumia muda mchache mtandaoni. | **Chini** |
| 2009 – 2017 | Mpangilio wa kuchapisha kwa kufuata wakati katika nafasi ya pamoja unazidi kubadilishwa polepole na uchujaji wa maudhui wa **kialgorithimu unaofuata** vigezo vya siri (Facebook mwaka 2009; Instagram na Twitter mwaka 2016). | **Kati:** Maudhui hupangwa upya kulingana na algorithms za siri. Utafiti unaonyesha kuwa watumiaji wengi hawakuwa na ufahamu kuhusu mchakato wa uchujaji wa maudhui. | **Kati:** Idadi ya watumiaji duniani hufikia bilioni 2.46 mwaka 2017. Kwa wastani, watumiaji hutumia dakika 128 kwa siku kwenye mitandao ya kijamii. | **Kati** |
| 2017 – 2020 | Ufunuo wa taratibu kwa maudhui ambayo hayajaandikwa wala kushirikiwa na watu ambao mtumiaji ameamua kuwafuata: Inatosha mtu yeyote awe amerejea au kupenda maudhui hayo (kama “like” ya Twitter au Facebook, badala ya Share au Retweet).Mfumo wa “Hadithi” wa Snapchat unapanuka: **majukwaa yanahamisha kiotomatiki mtumiaji kwenda kwenye hadithi inayofuata baada ya sekunde chache zilizowekwa.** | **Upana:** Algoritimu zinapata uhuru wa kufanya maamuzi, zikifanya kazi katika ulimwengu mpana zaidi wa maudhui. Hii inasababisha kuongezeka kwa nafasi inayodhibitiwa na upangaji wa kialgoritimu ndani ya jukwaa, na wasimamizi wanapata udhibiti juu ya kipengele cha muda. | **Juu:** Idadi ya watumiaji yafikia bilioni 2.9. Kwa wastani, kila mtumiaji hutumia dakika 145 kwa siku kwenye mitandao ya kijamii. | **Juu** |
| 2020 – Today | **Watumiaji wanaonyeshwa maudhui yanayotolewa na mtumiaji yeyote wa jukwaa.** Kwa kukua kwa mtindo wa TikTok, uendelezaji wa moja kwa moja wa maudhui unapata nafasi zaidi. | **Pana sana:** Ulimwengu wa maudhui ambao algoriti huchagua kile cha kumuonyesha kila mtumiaji hauwekewi tena mipaka na mtandao wa watu ambao kila mtumiaji ameamua kuwafuata. | **Juu sana:** Idadi ya watumiaji inafikia bilioni 4.7 (2022). Kwa wastani, kila mtumiaji hutumia dakika 147 kwa siku kwenye mitandao ya kijamii. | **Juu Sana:** |

Chanzo: Kimeandaliwa na mwandishi kwa kuzingatia vyanzo mbalimbali.

Maelezo haya kuhusu ongezeko la mamlaka yanayotekelezwa na kampuni za mitandao ya kijamii juu ya nyanja ya habari duniani ni mfano wa wazi sana wa mchakato mpana wa kuunganishwa kwa mamlaka katika mazingira ya kidijitali. Kwa upande mwingine, muunganiko huu wa mamlaka katika sekta ya makampuni ni sehemu ya mwelekeo mpana zaidi ambapo maamuzi mengi muhimu ambayo hapo awali yalikuwa chini ya viongozi waliowekwa madarakani kidemokrasia sasa yako mikononi mwa kundi dogo lisilowajibika la makampuni binafsi.

**Ukuaji wa mamlaka ya makampuni yasiyozuiliwa:** Mazingira ya kiteknolojia ya sasa yanazidi kuwa magumu kufahamika, huku ugumu mkubwa wa kiteknolojia ukiambatana na tafsiri kandamizi za sheria zilizopo za ulinzi wa mali miliki pamoja na matumizi ya kupita kiasi ya mikataba ya kutofichua taarifa (non-disclosure agreements). Muktadha huu unadhoofisha kwa kiasi kikubwa uwezo wa taasisi na mifumo yetu mingi ya sasa kutimiza lengo lake la kuhakikisha kwamba maendeleo ya kiuchumi na kiteknolojia yanatekelezwa kwa kuzingatia maslahi ya umma na haki za watu.

Mabadiliko haya yanaweza kuhitaji mashirika ya kiraia kufikiria upya mbinu zao za kushirikiana na mashirika ya serikali pamoja na makampuni. Hasa, hali hii inahitaji umakini zaidi kuhusu kiwango ambacho ufadhili kutoka kwa makampuni unaunda na kuathiri mjadala na ajenda ya haki za kidijitali katika miaka ijayo.

## C. MIELEKEO

### 1. KUUNGANISHWA KWA NGAZI ZOTE ZA MIUNDO YA MTANDAO

Intaneti, barua pepe, na wavuti zilibuniwa kufanya kazi kwa kutumia itifaki ya wazi. Hii iliwezesha mfumo wa taarifa usio na kituo kimoja kuu kuibuka na kubaki imara na bunifu. Katika miongo iliyopita, ngazi kadhaa muhimu za mifumo hii zimekuwa zikijikumulisha zaidi na zaidi. Matokeo yake ni mazingira ambayo hayabuni mambo mapya kwa urahisi, yanayoweza kusababisha matatizo makubwa pindi yanaposhindwa, na yanayoweza kudhibitiwa kwa urahisi na wamiliki wa nguvu wa zamani na wapya, iwe ni makampuni makubwa ya kimataifa au serikali zinazolinda nafasi zao za udhibiti wa soko.

*Mchoro 4 Mchoro wa usanifu wa mtandao (kulingana na Baran, 1962)*



**Kuunganishwa kwa Tabaka la Hifadhi na Usindikaji wa Data:** Amazon, Microsoft, na Google kwa sasa wanadhibiti zaidi ya 65% ya soko la huduma za wingu (cloud computing)[39]. Idadi ya huduma zinazotegemea wingu inaendelea kuongezeka, na kuunganishwa kwa programu za akili bandia (AI) ambazo zinahitaji seti kubwa za data kwa ajili ya mafunzo na nguvu kubwa ya usindikaji kunaonekana kuendeleza mwelekeo huu zaidi. Mchakato huu unatufikisha tena kwenye hatua za awali za kompyuta, ambapo uwezo wa usindikaji ulikuwa mahali pamoja (kituo kikuu), na mtumiaji wa kawaida alitumia kifaa kisicho na uwezo mkubwa (terminal isiyo na akili). Pia, mwelekeo huu unazidisha ukosefu wa usawa wa kijiografia: Wakati asilimia 43 tu ya trafiki ya kimataifa kutoka nchi za Ulaya huenda Marekani (na iliyosalia kwenda katika nchi nyingine za Ulaya), kwa upande wa Amerika ya Kusini takriban asilimia 73 ya trafiki ya kimataifa huenda Marekani. Katika Afrika, asilimia 32 ya trafiki huenda kwenye seva zilizopo Ulaya, huku asilimia 56 ikiishia Marekani[40].

Njia nyingine ya kutathmini uwekaji wa miundombinu ya seva ni kwa kuangalia idadi ya seva salama kwa kila watu milioni moja. Seva salama zinaweza kutumika kama kiashiria cha upana wa miundombinu ya upangishaji iliyopo katika nchi au kanda fulani. Kama grafu hapa chini inavyoonyesha, maeneo mengi ya Kusini mwa Dunia yamekuwa yakiongeza uwezo wao kwa miaka, isipokuwa Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, ambako ukuaji huo umesimama kati ya 2017 hadi 2020. Hata hivyo, ikilinganishwa na nchi zilizo katika kitovu cha kiuchumi, ukuaji huu ni mdogo sana, jambo ambalo linaweza kueleza na kuendeleza mwelekeo ulioelezwa hapo juu. Pengo kati ya Marekani/Ulaya na maeneo mengine ni kubwa sana kiasi kwamba kuwaweka kwenye grafu moja kunafanya maeneo ya Kusini mwa Dunia yaonekane kana kwamba hayapo kabisa[41]. Kwa sababu hizi, Marekani na EU wameondolewa kwenye grafu hapa chini. Kwa marejeleo: ingawa Amerika ya Kusini na Karibiani (inayoongoza kwenye grafu hapa chini) ilionekana kuwa na seva salama 1,969 kwa kila watu milioni moja mwaka 2020, EU ilikuwa na 50,266 na Marekani 140,804 kwa mwaka huo huo.

*Mchoro 5. Severi salama kwa kila watu milioni moja*[42]




Chanzo: Imetengenezwa na mwandishi kwa kutumia data kutoka netcraft.com na makadirio ya idadi ya watu ya Benki ya Dunia.

**39.** Mark Haranas, "AWS, Microsoft, Google's Cloud Market Share Q1 2023," CRN (blog), 4 Mei 2023, https://www.crn.com/news/cloud/aws-microsoft-google-s-cloud-market-share-q1-2023.

**40.** Telegeography, "Global Internet Map Map 2018," 2018, https://global-internet-map-2018.telegeography.com/. Kwa data kuhusu eneo la MENA, tazama https://store.rationalstat.com/store/middle-east-north-africa-data-center-market-analysis-forecast/.

**41.** See https://data.worldbank.org/indicator/IT.NET.SECR.P6?locations=ZQ-EU-ZJ-IN-ZG-Z4-US.

**42.** Hii inarejelea idadi ya vyeti tofauti vya TLS/SSL vinavyoaminiwa hadharani vilivyopatikana katika Utafiti wa Netcraft wa Seva Salama. Mahali pa eneo linaweza kufuatwa kutoka kwa mahali pa mwenyeji wa tovuti zinazotumia vyeti hivyo (badala ya nchi zilizoonyeshwa kwenye vyeti wenyewe). Maelezo zaidi kuhusu mbinu ya utafiti yanapatikana katika https://data.worldbank.org/indicator/IT.NET.SECR.P6?locations=ZQ-EU-ZJ-IN-ZG-Z4-US.

Takwimu hizi zinaangazia ukosefu wa miundombinu ya hifadhi ya data katika maeneo kama Afrika na Amerika ya Kusini, pamoja na kuwepo kwa usanifu wa mtandao wa aina ya “hub and spoke”, ambapo vituo vya mamlaka vinatenda kama kitovu cha taarifa ambacho husambaza taarifa hizo duniani kote. Nchi zilizoko pembezoni huunganishwa hasa kupitia vituo vilivyoko katika Umoja wa Ulaya na Marekani, ambavyo hupata mamlaka ya kudhibiti ufikiaji wa taarifa.[43] Mwelekeo huu unazuia uwezo wa serikali kutoka katika nchi nyingi za ulimwengu wa walio wengi kuunda mazingira bora ya kisheria, kwani ukosefu wa miundombinu unamaanisha pia upungufu wa ujuzi wa kitaifa, maarifa ya ndani, au zana za kuhakikisha utekelezaji wa sheria unafanyika ipasavyo. Kama ilivyofichuliwa na Edward Snowden, hali hii pia hufanya maeneo hayo ya udhibiti wa taarifa kuwa rahisi kutumiwa vibaya kwa ajili ya ujasusi.

**Mjikumuliko katika safu ya usafirishaji wa data:** Usafirishaji humaanisha nyaya (kebo) zinazounganisha seva duniani kote. Hapa tunaweza kuona kuwa ongezeko kubwa la uwezo wa usafirishaji linachochewa na uwekezaji kutoka kwa kampuni chache binafsi zinazojishughulisha na uzalishaji na usimamizi wa maudhui. Hii inaonyesha kuwa mjikumuliko (centralization) hautokei tu ndani ya safu au tabaka moja, bali ni sehemu ya mchakato wa ujumuishaji wa wima (vertical integration). Mnamo mwaka 2019, ilikadiriwa kuwa asilimia 70 ya ongezeko la upana wa njia wa kimataifa (bandwidth) duniani kote kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita lilitokana moja kwa moja na kampuni za watoa maudhui kama Microsoft, Google, Facebook na Amazon, ambazo tayari zilikuwa zinadhibiti zaidi ya asilimia 50 ya uwezo wa kebo za chini ya bahari, mara nyingi kupitia umiliki wa kipekee wa nyaya hizo.[44]

**Ujumuishaji katika tabaka la maudhui:** Tukilitumia wavuti kama mfano wa safu ya maudhui, tunaweza kuona kwamba Google imefanikiwa kudhibiti asilimia 65 ya soko la vivinjari vya wavuti duniani kupitia Google Chrome, ikifikia asilimia 74 barani Afrika, asilimia 78 Amerika Kusini[45] na asilimia 87.5 nchini India[46].




**43.** Tazama https://global-internet-map-2018.telegeography.com/ and https://www.theguardian.com/world/interactive/2013/nov/01/prism-slides-nsa-document.

**44.** Adam Satariano et al., “How the Internet Travels Across Oceans (Published 2019),” *The New York Times*, 10 Machi, 2019, sec. Technology, https://www.nytimes.com/interactive/2019/03/10/technology/internet-cables-oceans.html.

**45.** StatCounter, “Browser Market Share Worldwide,” StatCounter Global Stats, Novemba 2023, https://gs.statcounter.com/browser-market-share.

**46.** StatCounter, “Browser Market Share India,” StatCounter Global Stats, 2023, https://gs.statcounter.com/browser-market-share/all/india.

Mtafutaji wa Google unaomilikiwa na kampuni mama Alphabet unadhibiti asilimia 92 ya soko la utafutaji duniani kote, ukifikia asilimia 95 katika Amerika Kusini[47], na asilimia 98 barani Afrika na nchini India[48].




Kwa kuunganisha na udhibiti wa Alphabet juu ya mfumo wa uendeshaji wa Android, ambao unashikilia asilimia 70 ya soko la simu za mkononi duniani, hali hii inafikia asilimia 83 katika Amerika Kusini[49], asilimia 85 barani Afrika, na asilimia 95 nchini India[50].




Udhibiti huu unaipa kampuni mama, Alphabet, nafasi ya kipekee ya kuchunguza kwa undani mtandao mzima wa miunganisho kati ya vipande vya taarifa vinavyoundwa na watumiaji wa wavuti. Aidha, unawapa uwezo wa kuathiri matokeo ya soko na mtiririko wa taarifa. Alphabet imefikia kiwango cha juu sana cha udhibiti wa wavuti kiasi kwamba inakadiriwa kuwa idadi ya mibofyo (clicks) ya kila mwezi kwenye YouTube na Google kwa pamoja inazidi mibofyo yote ya tovuti 48 zinazofuatia kwa umaarufu[51]. Hivyo basi, Alphabet inashikilia mamlaka makubwa juu ya uhuru wetu wa kupata maarifa na kujieleza.

